Sikika

Jarida la Sikika

Namba ya Usajili -00005809 Toleo 2: Juni, 2011

"Utetezi wa Sera na Utawala Bora Katika Sekta ya Afya"

Utangulizi

Na Eugenia Madhidha

KARIBU katika toleo la pili la jarida la Sikika lenye lengo la kuelezea na kufafanua shughuli zetu na matukio mbalimbali yaliyojiri katika sekta ya afya. Bila shaka makala zetu zitakuwa na msaada mkubwa kwako mpendwa msomaji. Karibu, furahia jarida letu na tutafurahi kupata maoni zaidi toka kwako msomaji.

Katika robo hii ya pili ya mwaka 2011 shirika limekuwa katika mchakato wa kuanzisha kituo cha redio jamii mkoani Dodoma. Lengo la kuanzisha kituo hiki ni kuboresha uhusiano kati ya watunga sera, watoa huduma na wananchi kwa ujumla hususan katika masuala ya afya. Redio hii itawapa fursa mbalimbali wananchi kuchangia mada zinazohusiana na masuala ya afya na pia itatoa nafasi kwa wananchi kueleza matatizo wanayokutana nayo na kutoa maoni yao kwa watoa huduma na watunga sera jinsi ya kuboresha huduma za afya. Mchakato wa usajili na maandalizi umeshaanza na kituo kinatarajiwa kuanza kurusha matangazo yake siku za karibuni.

Kwa mujibu wa mpango mkakati wetu tayari shirika limeshaanza kufanya kazi mkoani Dodoma kwenye wilaya za Mpwapwa na Kondoa. Katika wilaya hizi, Sikika ilianza shughuli zake kwa kukutana na wadau mbalimbali wanaofanya kazi katika sekta ya afya. Pia tulipata fursa ya kujadili kwa pamoja na watendaji wa serikali wa nyanja mbalimbali katika sekta hiyo. Lengo likiwa jinsi gani tunaweza kushirikiana kwa pamoja ili tuweze kuboresha huduma bora za afya katika vituo vyetu vya huduma.

Kipindi cha mwezi Juni kila mwaka ni muhimu sana kwa watanzania. Kipindi hiki ndio kinachowafahamisha watanzania walio wengi

Jengo la Ofisi ya Sikika mikoani Dodoma likiwa katika matayarisho ya hatua za mwisho. Makao makuu ya Tija FM yatakuwa pia kwenyeofisi hii.

mwelekeo wa mapato na matumizi ya serikali kwa kipindi cha mwaka wa Fedha 2011/2012. Kwa Sikika, mwezi huu ni muhimu sana kwetu kwani ni mwezi ambao tunafuatilia kwa ukaribu sana utekelezaji wa ahadi za wizara ya afya katika kutimiza malengo ya kupungunza matumizi yasiyo ya lazima na jitihada za kuboresha huduma za afya nchini kwa kutoa kipaumbele kwenye bajeti katika sekta ya afya. Kwa kipindi hiki Sikika ilifanikiwa kutumia mitandao yake ya Twitter na Facebook katika kukuza mijadala mbalimbali katika sekta ya afya.

Ili kufahamu undani wa kazi tulizozifanya kwa robo hii ya pili ya mwaka tafadhali endelea kusoma makala zetu kama zilivyoandikwa na waandishi wetu.

Kwa taarifa zaidi usisite kutembelea tovuti yetu www.sikika.or.tz na kwa maoni yoyote tafadhali tutumie kwa barua pepe: info@sikika.or.tz

NDANI

Benki ya Dunia na Mpango wa Kuziwezesha AZAKI..... 2
Serikali yapunguza matumizi yasiyo ya lazima..... 2
Maadili kazini ni nyenzo muhimu katika kuleta huduma bora..... 3

Benki ya Dunia na Mpango wa Kuziwezesha AZAKI

Na Scholastica Lucas

KUTOKANA na mchakato wa kuondokana na upungufu wa dawa na vifaa tiba katika jumuiya ya Afrika Mashariki ulioanza hivi karibuni, Benki ya Dunia imeanzisha mpango wa kuimarisha usimamizi katika ununuzi wa bidhaa za dawa. Mpango huu utawezesha ushiriki wa Asasi Za Kiraia (AZAKI) katika kuboresha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa manunuzi ya dawa na vifaa tiba hususani kwa vituo vya huduma za afya vya umma.

Aidha, mpango huu unajumuisha maandalizi ya vifaa vya ufundishaji na uwezeshaji kama vile vitini vya mafunzo ambavyo kwa sasa vipo katika hatua za maandalizi ya awali. Vitini hivi vinaandaliwa na jopo la wataalamu wa masuala ya dawa na vifaa tiba, Sikika ikiwa ni mmoja washiriki wa jopo hilo. Mchakato huu ulianza rasmi kwa warsha ya siku tatu iliyofanyika Dar es salaam kuanzia tarehe 22 hadi 24 Juni, 2011.

Kwa ujumla vitini hivyo vinalenga kutoa elimu ya mchakato mzima wa ununuzi wa dawa na vifaa ambapo AZAKI za afrika mashiriki ni moja kati ya walengwa. Huu utakuwa mwanzo mzuri kwa AZAKI kama Sikika kushiriki kikamilifu katika kusimamia michakato ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba ili kuboresha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya huduma za afya vya umma.

Picha ya pamoja ya wataalamu walioshiriki kutengeneza kitini cha mafunzo kwa ajili ya kufundishia Asasi za kiraia juu ya mchakato wa manunuzi na usambazaji wa dawa na vifaa tiba

Hivyo, Sikika inafurahia mpango huu kwa kuwa unasaidia AZAKI kushiriki karika kuboresha ufanisi na uwajibikaji katika ununuzi wa dawa na hivyo kuondokana na adha ya upungufu wa dawa na vifaa tiba ambayo imekuwa ni changamoto kubwa kwa sekta ya afya nchini na barani Afrika kwa ujumla.

Serikali yapunguza matumizi yasiyo ya lazima

Na Eva Emmanuel

KATIKA nusu ya kwanza ya mwaka 2011 Sikika ilitetea ongezeko la ufanisi katika bajeti ya sekta ya afya katika ngazi ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Ili kufikia lengo hili shirika lilifanya utafiti kwa kuchambua bajeti za wizara zote, Idara na Wakala wa Wizara, na, hesabu za Mikoa huku tukiweka kipaumbele katika matumizi yasiyo ya lazima ambayo hujumuisha posho za ziara za mafunzo ndani na nje ya nchi, takrima, ununuzi wa magari na vitu vinavyoambatana na hili kama vile mafuta ya kulainishia mitambo na mafuta ya kuendeshea. Lengo la utafiti lilikuwa kujua iwapo serikali inapunguza matumizi yasiyo ya lazima na kuelekeza rasilimali katika maeneo yenye tija.

Katika mwaka huu wa fedha, uchambuzi wetu kuhusiana na bajeti za mikoa umebainisha kwamba serikali chini ya ofisi ya Waziri Mkuu imefanikiwa kupunguza bajeti ya matumizi yasiyo ya lazima yaliyotajwa hapo juu ambayo

Sikika na Wajumbe wa kamati wakibadilisha uzoefu katika masuala ya bajeti ya afya ikiwa ni wiki mbili kabla ya kikao cha bunge kuanza mjini Dodoma. Mkutano huo ulifanyika katika ukumbi wa City Paradise Hotel Benjamini Mkapa Tower Mei 29, mwaka huu.

hayana athari kubwa kimaendeleo. Kiasi cha Shilingi bilioni 30 zimetengwa kwa ajili ya matumizi yasiyo ya lazima kiasi ambacho ni pungufu ya kile cha miaka miwili ya fedha iliyopita ambapo serikali kwa mwaka wa fedha 2009/2010 ilitenga Shilingi bilioni 55.6 na bilioni 38 kwa mwaka 2010/2011.

Kupungua kwa matumizi haya kunathibitishwa na kupunguza ununuzi wa magari mapya ya serikali ambapo kiasi cha fedha zilizotengwa zilishuka kutoka shilingi bilioni 2.9 mwaka wa fedha uliopita (2010/2011) hadi shilingi bilioni 1.1 mwaka huu wa fedha 2011/2012. Mafanikio haya yamefikiwa kwa sababu mikoa 14 kati ya 21 haikutenga fedha za ununuzi wa magari. Pia, mikoa iliyotenga fedha za ununuzi wa magari ilitenga kiasi kidogo kisichotosha kununulia magari ya bei ghali na ya kifahari. Kwa mfano Tabora na Ruvuma ilitenga shilingi milioni 5 na milioni 6.7 kwa ajili ya ununuzi wa magari.

Aidha, serikali imefanikiwa kupunguza gharama za mafunzo na ziara. Katika mwaka wa fedha 2010/11 na 2011/12, bajeti ya mafunzo nje ya nchi imeshuka kutoka shilingi bilioni 280 hadi shilingi bilioni 155 na bajeti ya ziara za nje ya nchi imepunguzwa kutoka shilingi milioni 415 hadi shilingi milioni 353.

Matokeo ya utafiti huu yaligawiwa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, wafadhili na jopo la Wizara ya Afya. Aidha, Sikika ilitoa taarifa kwa vyombo vya habari ikipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa utekelezaji wa ahadi zake. Pia, matokeo yatasambazwa kwa wananchi ili waweze kuendelea kufuatilia utekelezaji wa mipango ya serikali na hatimaye kuweza kuiwajibisha serikali pale ambapo matumizi ya kodi za wananchi yanapokuwa hayajatumika katika kuleta tija hasa kwenye huduma za afya nchini.

Maadili kazini ni nyenzo muhimu katika kuleta huduma bora

Lydia Kamwaga na Godwin Kabalika

HUDUMA bora za Afya ni moja ya mahitaji muhimu ya binadamu katika maisha yake ya kila siku. Moja ya kipaumbele cha serikali na hata wafadhili na asasi za kiraia nchini ni suala zima la afya.

Ni dhahiri kwamba bila afya bora katika taifa lolote duniani hakuna maendeleo. Ni ukweli usiopingika kuwa upatikanaji wa huduma bora katika eneo lolote lile kunategemea sana uzingatiaji wa maadili kwa watoa huduma wa eneo hilo.

Katika kulitekeleza suala hilo Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kupitia Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) ilitunga kanuni za maadili ya utendaji kazi katika utumishi wa umma ili kuhakikisha huduma zinatolewa ipasavyo katika sekta ya afya,Sikika inaamini kuwa uzingatiaji wa maadili ya wafanyakazi wa afya ni moja ya nguzo muhimu katika kuboresha huduma hizo hapa nchini.

Sikika imefanya tafiti mbalimbali za ufuatiliaji wa masuala ya maadili katika wilaya tatu za mkoa wa Dar es Salaam, Kibaha (Pwani), Mpwapwa

na Kondoa (Dodoma). Matokeo ya tafiti yanaonyesha kwamba kuna udhaifu mkubwa katika kuzingati maadili miongoni mwa watoa huduma za afya. Tatizo hili la ukosefu wa uadilifu limelalamikiwa na wananchi walio wengi katika jamii husika jambo ambalo limeonekana kwa kiasi kikubwa kuathiri utoaji wa huduma za afya.

Ingawa kumekuwa na kauli mbiu mbalimbali zinazokemea utovu wa maadili kazini kama vile 'zingatia maadili pambana na rushwa,' 'Pambana na rushwa ili kuimarisha utawala bora', ukosefu wa maadili miongoni mwa watoa huduma bado umeendelea kukithiri.

Tafiti zinabainisha kuwa kwa kiwango kikubwa, huduma za afya zimeendelea kuwa si za kuridhisha nchini. Na pia takwimu za vifo vya akina mama na watoto zinaendelea kuwa juu na vifo vinavyotokana na magonjwa yanayotibika kutopungua. Sikika inaamini kuwa hali hii inachangiwa na ukiukwaji wa maadili ya watoa huduma hizi. Utafiti umeonesha kuwa wananchi wengi hawaridhishwi na maadili ya watumishi wa afya katika vituo vya huduma.

Changamoto kubwa inayosababisha baadhi ya matatizo haya miongoni mwa watumishi wa afya ni kuwepo kwa tabia za rushwa, unyanyapaa kwa wagonjwa pindi wanapotaka huduma, ulevi wakati wa kazi pamoja na kufanya kazi kwa kupendelea ndugu au rafiki. Mambo haya yote ni kinyume na kanuni za maadili ya utendaji katika utumishi wa umma kama yalivyoainishwa na Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma).

Aidha, baadhi ya mambo yaliyoainishwa katika kanuni hizo ni pamoja na kutoa huduma bora ya afya na kufanya kazi bila upendeleo wa aina yoyote, kufanya kazi kwa uadilifu pamoja na kuwajibika kwa umma (URT, 2005).

Sikika inatoa wito kwa wananchi wote kushiriki katika kuhakikisha kuwa suala la maadili ya kazi linazingatiwa. Hili si suala la serikali peke

Baadhi ya wananchi wa kata ya Pwaga Wilaya ya Mpwapwa wakifuatilia maelezo juu ya viashiria vya maadili ya watumishi wa afya

yake, bali ni jukumu la jamii nzima. Hivyo jamii inapaswa itimize wajibu wake kwa kufikisha malalamiko yao juu ya tabia za ukiukwaji wa maadili katika vyombo husika ikiwa ni pamoja na kwenye masanduku ya maoni, vyumba vya kutolea maoni vilivyopo katika maeneo mbalimbali ya kutolea huduma za afya, kwenye ofisi za watendaji na uongozi wa kata, kwenye mikutano mbalimbali ya jamii, kwa mganga mkuu mfawidhi wa kituo husika pamoja na kupitia namba maalumu ya ujumbe mfupi wa maneno ya Sikika (0688 493882).

Sikika inapendekeza kwamba wadau mbalimbali katika sekta ya afya, ikiwemo serikali wapitie upya adhabu zilizopo za kuwawajibisha watumishi wasiozingatia maadili yao ya kazi kwa lengo la kuziboresha. Pia kuwepo na mbinu zitakazowawajibisha watumishi wa afya ili kuboresha huduma za afya kwa pamoja.

Kadhalika, watumishi wote wa umma wanaowajibu wa kufanya kazi kwa kufuata kanuni za maadili ya kazi. Aidha mamlaka za nidhamu zinapaswa kusimamia utekelezaji wa kanuni za maadili ya kazi katika utumishi wa umma ili kuhakikisha kuwa kanuni hizo zinafuatwa na kila mtumishi ili kujenga nidhamu katika utendaji wa shughuli za serikali. ***Tukumbuke kuwa maboresho ya huduma za jamii yapo mikononi mwetu!***

Mhariri: Tuma Abdalla
Waandishi:
Eugenia Madhidha
Scholastica Lucas
Eva Emmanuel
Lydia Kamwaga na Godwin Kabalika

P.O.Box 12183, Dar es Salaam
Tel: +255 222 666355/57, Fax: +255 222 6668015
Email: info@sikika.or.tz Website: www.sikika.or.tz